# TANZANIA NATIONAL ROADS AGENCY

P.O Box 11364
3rd Floor
Maktaba Complex
Bibi Titi Mohamed Road
Dar es Salaam

Tanzania National Roads Agency
TANROADS
Good roads for national development

**Tarehe** 10-September-07

**Kumbukumbu** TRD/D/GEN/P.43/VOL.II/

Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
(Uwaba)
SLP 12247
**Dar es Salaam.**

---

**YAH: TAARIFA KUHUSU USANIFU WA BARABARA ZINAZOJENGWA KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM**

Tafadhali rejea barua yako ya tarehe 15 Juni 2007 kuhusu somo tajwa hapo juu ambayo imetutaka kutoa ufafanuzi wa hoja za usanifu wa barabara zetu hapa nchini na hasa katika Jiji la Dar Es Salaam

Hoja zilizowasilishwa zimezingatia zaidi barabara za sam nujoma, Nelso Mandela na barabara ya Kilwa ambazo ziko katika hatua mbalimbali za kiutekelezaji.

Kwa barua hii ninakutumia majibu ya maswali ya hoja husika kama ilivyoambatanishwa.

Kuhusu maombi ya chama kutaka kukutana na uongozi wa (TANROADS) ili kuwasilisha na kuzungumzia hoja za kiusalama wa watumia barabara, maombi hayo yamezingatiwa na tutawafahamisha siku ya kukutana baada ya kukamilisha maandalizi husika.

Napenda kutumia fursa hii kuushukuru uongozi wa chama cha wapanda baiskeli kwa maamuzi makini ya kushirikiana nasi katika suala zima la kuboresha matumizi ya barabara zetu hasa katika suala la usalama.

Tunaahidi kuendeleza ushirikiano na chama chenu.

Asante sana.

Ephraem C M Mrema
**MTENDAJI MKUU**

S.J.M

**Majibu ya wa panda baisikeli UW ABA**

1. **Swali**

   Kwenye barabara hii imepangwa wapi baisikeli za kawaida,baisikeli za walemavu,maguta,mikokoteni,watembea kwa miguu na magari zitapita? Kuna nafasi gani kwenye barabara kwa aina hizi zote za usafiri? Wote wapite sehemu moja au kuna sehemu hasa kwa aina mbali mbali za usafiri? Wapanda baisikeli wapite pamoja na watembea kwa miguu au pamoja na magari au kuna sehemu hasa kwa wapanda baisikeli?

   **Jibu**

   Usanifu wa barabara zetu umetenga sehemu mbadala za kupita vyombo vya moto vikiwemo Magari, Pikipiki, Maguta nk.Aidha njia ya usafiri wa vyombo vya baiskeli za kawaida na za walemavu pamoja na mikokoteni vimewekewa sehemu yake maalum ya kupita. Kwa upande wa waenda kwa miguu nao pia wamewekewa njia yao mbadala ili kutokuingiliana na vyombo hasa vya moto.

2. **Swali**

   Kila sehemu ya barabara ina Upana gani?

   **Jibu**

   Barabara hizi zimesanifiwa kulingana na viwango vya kimataifa kama ifuatavyo.
   (a) Sam Nujoma -Upana wa njia za magari ni meta 7, upana wa njia ya vyombo vya Baiskeli pamoja na mikokoteni ni meta 5 na upana wa njia ya waenda kwa miguu ni meta 2. Utaratibu huu utawekwa kwa kila upande wa barabara hii.

   (b) Barabara ya Nelsoni Mandela - Upana wa njia za magari ni meta 7.5, upana wa njia ya vyombo vya Baiskeli pamoja na mikokoteni ni meta 3. Utaratibu huu utawekwa kwa kila upande wa barabara hii.
   (C) Barabara ya kilwa - Vpana wa njia za magari ni meta 7.5, upana wa njia ya vyombo vya Baiskeli pamoja na mikokoteni ni meta 3 na upana wa njia ya waenda kwa miguu ni meta 3. Utaratibu huu utawekwa kwa kila upande wa barabara hii.

3. **Swali**

   Kuna mipango gani ya vituo vya mabasi? Baisikeli zitapita vipi vituo vya mabasi- nyuma au mbele?

   **Jibu**

   Katika barabara hizi kutawekwa vituo vya mabasi. Aidha ilikuhakikisha usalamama wa wapanda baisikeli, watumiaji baiskeli watapita nyuma ya vituo vya mabasi kiasi kwamba hakutakuwa na mwingiliano wa watu wanosubiri magari katika vituo vya mabasi na wapanda baisikeli.

4. **Swali**

   Kuna mipango gani kwa barabara ndogo ambazo zinaingia kwenye 'plots' zilizo karibu na barabara kuu? Vipi watu wataingia na kutoka bila kusumbua wengine kwenye barabara?

   **Jibu**

   Barabara ndogo ambazo zinaingia kwenye 'plots' zilizo karibu na barabara kuu zitaunganishwa moja kwa moja kwenye service road ambayo itakusanya magari kuto kwenye Plots na kuyaelekeza barabar kuu ili kuendelea na safari zake.

5. **Swali**
Kuna mipango gani ya makutano ya barabara?

**Jibu**
Makutano yote ya barabara yamefanyiwa utafiti ili kubaini idadi ya magari kwa saa kwa kila makutano ya barabara husika. Katika makutano haya kutawekwa mifumo ya kiusalama ya kuongoza magari. Aina ya mifumo ya kuongoza magari itategemea wingi wa magari wa makutano husika. Mifumo ya usalama ya kongoza magari tuliyonayo kwa sasa kulingana na viwango vya kimataifa ni pamoja na Taffic light, Mzunguko (Round about) pamoja na barabara zajuu fly overs.

6. **Swali**
Vi pi watembea kwa miguu na wapanda baisikeli watalindwa wasigongwe,na kuna kingo gani kulinda sehemu za watembea kwa miguu na baisikeli ili magari yasiingie kupaki au kupita foleni?

**Jibu**
Alama za kiusalama na tahadhali kwa watumiaji barabara (roads signs') zitawekwa kulingana na mahitaji na viwango vilivyopo. Njia za watembea kwa miguu (footpath) zitakingwa kwa tofali ngumu za zege (kerbstones) ambazo zitazuia magari yasiingie au kupaki katika njia hizi.

7. **Swali**
Kuna mpango gani wa upandaji wa miti?

**Jibu**
Miti itapandwa kandokando ya njia za waenda kwa miguu 'service roads' kwa kushirikisha nguvu za wananchi kwani upandaji miti ni kampeni ya kitaifa.

8. **Swali**
Kuna mpango gani wa taa za barabarani?

**Jibu**
Taa za barabarani ni sehemu ya kazi ya mkataba wa ujenzi katika barabara hizLKwa hiyo zitawekwa kulingana na mahitaji na umuhimu wa barabara.